JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2024

## MAARIFA YA JAMII

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA MASWALI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2024

# 03 MAARIFA YA JAMII

Kimechapishwa na;

Baraza la Mitihani la Tanzania,

S.L.P 2624,

Dar es salaam, Tanzania.

**©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2024**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI .......... iv
1.0 UTANGULIZI .......... 1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA KILA SWALI .. 2
2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha .......... 2
2.1.1 Swali la 1: Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka na Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii .......... 3
2.1.2 Swali la 2: Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka .......... 12
2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi .......... 18
2.2.1 Swali la 3: Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali .......... 19
2.2.2 Swali la 4: Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku .......... 28
3.0 TATHIMINI YA UFAULU KWA KILA UMAHIRI .......... 34
4.0 HITIMISHO .......... 34
5.0 MAPENDEKEZO .......... 35
KIAMBATISHO: Ulinganifu wa Ufaulu kwa Wanafunzi katika kila Umahiri kwa Mwaka 2024 na 2023.. .......... 37

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne 2024 kwa somo la Maarifa ya Jamii. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, wathibiti ubora wa shule, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu kiwango cha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Msingi.

Katika taarifa hii, mambo yaliyochangia ufaulu wa wanafunzi katika kila swali yamebainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa, ufaulu mzuri wa wanafunzi katika maswali ulitokana na uelewa mzuri wa matakwa ya maswali na kuwa na umahiri wa kutosha katika somo. Aidha, wanafunzi waliokuwa na ufaulu hafifu katika upimaji huu hawakuwa na maarifa ya kutosha kutambua matakwa ya maswali. Wanafunzi wengine walikuwa na umahiri wa wastani katika umahiri uliopimwa.

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika kila umahiri unaonesha kuwa, ufaulu wa wanafunzi ni wa wastani katika umahiri ufuatao ambao ni: *Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali, Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii, Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka na Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku.*

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, mrejesho huu utaziwezesha mamlaka mbalimbali za elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha michakato ya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, Baraza linatarajia kuwa, changamoto zilizochangia ufaulu usioridhisha hususan katika umahiri wa *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku* zitatatuliwa ili kufikia ufaulu unaotarajiwa kwa wanafunzi wa Darasa la Nne.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukurani za dhati kwa wote walioshiriki katika kuandaa taarifa hii.



Prof. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2024 ulifanyika Oktoba 2024. Jumla ya wanafunzi 1,633,272 walisajiliwa kufanya upimaji katika somo la Maarifa ya Jamii. Kati yao, wanafunzi 1,530,382 (100%) walifanya upimaji ambapo, wanafunzi 1,374,134 sawa na alisimia 89.80 walifaulu na wanafunzi 156,144 sawa na asilimia 23.54 walipata ufaulu hafifu.

Katika taarifa hii, utangulizi unafuatiwa na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila swali. Uchambuzi unabainisha umahiri uliopimwa na majibu ya wanafunzi ambayo yamegawanyika katika kiwango kizuri, wastani na hafifu. Sababu za ufaulu kwa kila kundi pia zimechambuliwa. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila swali umefuatiwa na tathimini ya ufaulu wa wanafunzi katika kila umahiri. Sehemu hiyo imefuatiwa na hitimisho pamoja na mapendekezo yaliyotokana na uchambuzi uliofanyika.

Viwango vya ufaulu wa wanafunzi vimezingatia asilimia ya ufaulu wa swali husika. Iwapo asilimia ya ufaulu ni 0 hadi 33, kiwango cha ufaulu ni hafifu, iwapo asilimia ni 34 hadi 66, ufaulu huo ni wa wastani, na asilimia 67 hadi 100, kiwango cha ufaulu ni kizuri. Katika taarifa hii, rangi ya kijani, njano na nyekundu zimetumika kuonesha ufaulu mzuri, wastani na hafifu mtawalia.

Karatasi ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika mwaka 2024 somo la Maarifa ya Jamii ilikuwa na maswali manne. Maswali hayo yaligawanyika katika sehemu kuu mbili (A na B). Sehemu A ilikuwa na maswali mawili, swali la 1 na la 2 yenye

jumla ya vipengele 14. Maswali hayo yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii na Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka.*

Sehemu B iliundwa na maswali mawili, swali la 3 na la 4 yenye jumla ya vipengele 11. Maswali hayo yalitoka katika umahiri mkuu wa *Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali* na *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku.* Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu zote mbili.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA KILA SWALI

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa ujumla unaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu katika maswali yote kilikuwa cha wastani. Vielelezo na chati vimetumika kuonesha majibu ya wanafunzi na takwimu mtawalia.

### 2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua na Kuoanisha


Sehemu hii iliundwa na maswali mawili yenye jumla ya vipengele 14. Swali la 1 lilikuwa na vipengele nane (i) – (viii). Katika swali hili wanafunzi walitakiwa kusoma swali na kisha kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka katika machaguo waliyopewa na kuiandika herufi husika katika kisanduku walichopewa. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 16. Swali la 2 lilikuwa na vipengele sita (i) – (vi) vya kuoanisha, mwanafunzi alitakiwa kusoma maswali kutoka *Orodha A*, na kuoanisha na jibu sahihi kutoka *Orodha B.*

### 2.1.1 Swali la 1: Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka na Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii

Jumla ya wanafunzi 1,530,381 (100%) walijibu swali hili ambapo kati yao wanafunzi 8,335 (0.54%) walipata ufaulu mzuri sana kwa kuwa walijibu kwa usahihi vipengele vyote nane (8) na hivyo kupata alama 16. Wanafunzi wengine 108,025 (7.06%) waliopata alama kuanzia 12 hadi 14 waliweza kujibu kwa usahihi vipengele sita hadi saba katika swali hili na hivyo walipata ufaulu mzuri.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 826,094 (53.98%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 ambao ni ufaulu wa wastani. Kati yao, wanafunzi 178,203 (11.65%) waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vitano, wanafunzi 289,459 (18.91%) walijibu kwa usahihi vipengele vinne, na wengine 358,432 (23.42%) waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vitatu.

Hata hivyo, wanafunzi 587,927 (38.42%) walikuwa na ufaulu hafifu kwani walipata alama 0 hadi 4. Kati yao, wanafunzi 65,392 (4.27%) hawakujibu kipengele chochote, hivyo walipata 0. Wanafunzi wengine 196,138 (12.82%) walijibu kwa usahihi kipengele kimoja na wengine 326,397 (21.33%) walijibu kwa usahihi vipengele viwili. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani wanafunzi 942,454 (61.58%) walipata alama kuanzia 6 hadi 16 kama inavyoonekana kwenye Chati Na.1.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 1*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 1 umefanyika kama ifuatavyo:

(i) Kwa nini tarehe 25 Julai ya kila mwaka inakumbukwa Tanzania?

A Ni siku ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar

B Ni siku ya kumbukumbu ya mashujaa

C Ni siku ya uhuru wa Tanganyika

D Ni siku ya uhuru wa Zanzibar

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini tukio la kihistoria linalokumbukwa kila ifikapo tarehe 25 Julai nchini Tanzania. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *B, Ni siku ya kumbukumbu ya mashujaa.* Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matukio ya kihistoria yaliyotokea nchini Tanzania.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua vipotoshi *A, Ni siku ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar, C, Ni siku ya uhuru wa Tanganyika na D, Ni siku ya uhuru wa Zanzibar* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matukio ya kihistoria yaliyotokea nchini Tanzania. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa, siku ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni tarehe 26 Januari, Tanganyika ilipata uhuru tarehe 9 Disemba na uhuru wa Zanzibar ulipatikana tarehe 10 Disemba.

(ii) Sera ipi iliasisiwa na hayati Rais Benjamin William Mkapa?

A. Soko huria

B. Ubinafsishaji

C. Ujenzi wa viwanda

D. Ujamaa na kujitegemea

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini sera iliyoasisiwa na hayati Rais Benjamin William Mkapa. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sera husika, hivyo walichagua jibu sahihi *B, Ubinafsishaji*. Wanafunzi hao walitambua kuwa sera hiyo iliasisiwa na hayati Rais Benjamin William Mkapa.

Hata hivyo, wanafunzi waliochagua kipotoshi *A, Soko huria,* hawakuelewa kuwa, sera hiyo iliasisiwa na hayati Rais Ally Hassan Mwinyi. Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *C, Ujenzi wa viwanda,* walishindwa kuelewa kuwa, sera hiyo iliasisiwa na hayati Rais John Pombe Magufuli. Vivyohivyo, baadhi ya wanafunzi waliochagua kipotoshi *D, Ujamaa na*

*kujitegemea* walishindwa kuelewa kuwa sera hiyo iliasisiwa na hayati Mwl Julius Kambarage Nyerere.

(iii) Kiongozi yupi nchini Tanzania huteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa wabunge?

A Waziri Mkuu

B Spika wa Bunge

C Makamu wa Rais

D Jaji Mkuu

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini kiongozi anayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa wabunge nchini Tanzania. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *A Waziri Mkuu*. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mchakato mzima wa uteuzi wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hata hivyo, wanafunzi waliochagua kipotoshi B, Spika wa Bunge, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu namna Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anavyopatikana. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa Spika anachaguliwa na Wabunge kwa kura ya siri, miongoni mwa Wabunge au watu waliokidhi vigezo vya kuwa Mbunge kwa kufuata Katiba na Kanuni za Bunge.

Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *C, Makamu wa Rais,* hawakuelewa kuwa, sio lazima Makamu wa Rais ateuliwe miongoni mwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Makamu wa rais ni mgombea mwenza wa nafasi ya urais ambaye huteuliwa na chama chake cha siasa kabla ya uchaguzi mkuu kufanyika.

Vivyohivyo, wanafunzi waliochagua kipotoshi *D,* Jaji Mkuu*,* hawakutambua kuwa, Jaji Mkuu hapaswi kuteuliwa kutoka miongoni mwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, uchaguzi B, C na D kutokuwa sahihi katika swali hili.

(iv) Kwa nini Wajerumani walivamia Tanganyika mwaka 1886?

A Walihitaji masoko ya kuuza bidhaa za viwanda vyao

B Walitaka kuwaondoa Waarabu Tanganyika

C Waliwahitaji watu weusi kwenda kufanya kazi Ujerumani

D Walitaka kufufua utalii katika mbuga za Wanyama

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini kusudi la uvamizi uliofanywa na Wajerumani nchini Tanganyika mwaka 1886. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *A, Walihitaji masoko ya kuuza bidhaa za viwanda vyao*. Uchaguzi wa jibu hili unadhihirisha kuwa wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sababu ya Wajerumani kuvamia Tanganyika mwaka 1886.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wengine walichagua kipotoshi *B, Walitaka kuwaondoa Waarabu Tanganyika*, C, *Waliwahitaji watu weusi kwenda kufanya kazi Ujerumani, na* D, *Walitaka*

*kufufua utalii katika mbuga za wanyama,* wanafunzi hawa hawakuwa na uelewa juu ya sababu za wavamizi kuvamia nchi yetu hasa Wajerumani kuvamia Tanganyika mwaka 1886.

(v) Vita vya Majimaji vilisababishwa na nini?

A Unyonyaji uliofanywa na Waingereza

B Ukatili wa Wamatumbi dhidi ya Wajerumani

C Tamaa ya Kinjekitile kujaribu silaha zake

D Unyonyaji uliofanywa na Wajerumani

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini sababu iliyopelekea kutokea kwa vita vya Majimaji. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri ambapo wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *D, Unyonyaji uliofanywa na Wajerumani.* Wanafunzi hao walithibitisha kuwa na maarifa sahihi juu ya chanzo ama sababu iliyopelekea kutokea kwa vita vya Majimaji. Walielewa kuwa watu walipigana na wajerumani kwa sababu ya kunyang'anywa ardhi, kulazimishwa kufanya kazi na kunyanyapaliwa hivyo walikuwa wanadai haki yao.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua vipotoshi; *A, Unyonyaji uliofanywa na Waingereza, B, Ukatili wa Wamatumbi dhidi ya Wajerumani* na *C, Tamaa ya Kinjekitile kujaribu silaha zake* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sababu iliyopelekea kutokea kwa vita vya Majimaji. Wanafunzi hao walipaswa kutambua kuwa, vita vya Majimaji havikuwa dhidi ya Waingereza bali vilikuwa dhidi ya Wajerumani. Vilevile wanafunzi walipaswa kujua sababu kuu iliyosababisha kutokea kwa vita vya

Majimaji ilikuwa ni Unyonyaji uliofanywa na Wajerumani kwa Waafrika.

(vi) Njia ipi hutumika kupata taarifa za mashujaa katika jamii?

A Kuangalia misuli ya miili yao

B Kwa kupiga ramli

C Kwa kusoma na kusimuliwa

D Kwa kuishi na ndugu zao

Katika kipengele hiki mwanafunzi alitakiwa kubaini njia zilizotumika kupata taarifa za mashujaa katika jamii. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri, kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *C, Kwa kusoma na kusimuliwa.* Jibu hili linadhihirisha kwamba wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu njia zinazotumika kupata taarifa za mashujaa katika jamii.

Hata hivyo, wanafunzi wengine waliochagua vipotoshi A, *Kuangalia misuli ya miili yao, B, Kwa kupiga ramli* na D *Kwa kuishi na ndugu zao*, hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu njia zinazotumika kupata taarifa za mashujaa katika jamii. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kwamba kuangalia misuli ya miili yao, kupiga ramli na kuishi kwa ndugu zao haviwezi kumbainisha mtu kuwa ni shujaa. Kwani mashujaa ni watu wanaoongozwa na mioyo ya upendo na uzalendo katika jamii zao na taifa kwa ujumla.

(vii) Kwa nini Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anakumbukwa Tanzania?

A Aliruhusu ubinafsishaji

B Aliongoza harakati za kudai uhuru

C Alianzisha sera ya soko huria

D Aliruhusu uanzishwaji wa vyama vingi vya siasa

Katika kipengele hiki mwanafunzi alitakiwa kubaini sababu ya kukumbukwa kwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere nchini Tanzania. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi waliweza kuchagua jibu sahihi *B, Aliongoza harakati za kudai uhuru.* Hii inadhihirisha kuwa, wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu viongozi wa Kitanzania na michango yao katika taifa. Hivyo, waliweza kutambua kuwa kiongozi aliyeongoza harakati za kudai uhuru nchini Tanganyika ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua vipotoshi *A Aliruhusu ubinafsishaji,* walikosa maarifa kuhusu kiongozi aliyeanzisha ubinafsishaji nchini Tanzania. Walipaswa kuelewa kuwa alikuwa Hayati Rais Benjamin William Mkapa. Vilevile wanafunzi waliochagua kipotoshi *C, Alianzisha sera ya soko huria* hawakuwa na uelewa kuwa sera ya soko huria lilianzishwa na Hayati Rais Ali Hassan Mwiny*i*. Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi D, *Aliruhusu uanzishwaji wa vyama vingi vya siasa* hawakuwa na uelewa kuwa kiongozi aliyeruhusu

kuanzishwa kwa vyama vingi vya siasa nchini Tanzania alikuwa ni Hayati Rais Ali Hassan Mwinyi.

(viii) Yupi ni kiongozi wa shughuli za Serikali katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

A Spika wa Bunge

B Rais

C Mwanasheria Mkuu wa Serikali

D Waziri Mkuu

Kipengele hiki kilimtaka mwanafunzi kubaini kiongozi wa shughuli za Serikali katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri, kwani wanafunzi wengi walichagua jibu sahihi *D, Waziri Mkuu.* Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu majukumu mbalimbali ya viongozi wa kitaifa, hivyo waliweza kubaini kuwa waziri mkuu ndiye kiongozi mkuu wa shughuli za Serikali katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi *A Spika wa Bunge* hawakuelewa kuwa, Spika wa Bunge sio kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa spika ni kiongozi mkuu wa mhimili wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi *B, Rais,* hawakuwa na uelewa kuwa, Rais ni kiongozi mkuu wa nchi na sio kiongozi wa shughuli za Serikali katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Wanafunzi wengine waliochagua kipotoshi *C, Mwanasheria Mkuu wa Serikali,* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali hawezi kuwa kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mshauri mkuu wa shughuli zote za kiserikali zinazohusu sheria.

### 2.1.2 Swali la 2: Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka


Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka na umahiri mahususi wa *Kutumia elimu ya hali ya hewa katika shughuli za kila siku*. Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kuoanisha kazi ya vifaa vya kupima hali ya hewa katika Orodha A na vifaa husika katika Orodha B, kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano waliyopewa. Swali hili liliwapima wanafunzi uwezo wa kutambua kazi ya vifaa vinavyotumika katika upimaji wa hali ya hewa na lilikuwa na jumla ya alama 12. Swali lilikuwa kama ifuatavyo:

Jibu kipengele cha (i) – (vi) kwa kuoanisha kazi ya vifaa vya kupima hali ya hewa katika **Orodha A** na vifaa husika katika **Orodha B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| **Orodha A** | **Herufi** | **Orodha B** |
|---|---|---|
| (i) Kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua. | (    ) | A Kipimajoto |
| (ii) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi. | (    ) | B Kipima mvua |
| (iii) Kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa. | (    ) | C Haigromita<br>D Baromita |
| (iv) Kifaa kinachotumika kupima unyevuanga. | (    ) | E Anemomita<br>F Kipimaupepo |
| (v) Kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo. | (    ) | G Stevenson screen<br>H Kampbeli Stok |
| (vi) Kifaa kinachotumika kupima uelekeo wa upepo. | (    ) | |

Kati ya wanafunzi 1,530,381 (100%) waliofanya swali hili, wanafunzi 122,790 (8.03%) walipata alama zote 12 ambao ni ufaulu mzuri sana. Wanafunzi 200,046 (13.07%) walipata alama 8 hadi 10 ambao ni ufaulu mzuri. Hata hivyo, wanafunzi wengine 582,198 (38.04%) walipata alama 4 hadi 6 ambao ni ufaulu wa wastani. Kwa upande mwingine wanafunzi 625,347 (40.86%) walikuwa na ufaulu hafifu kwani walipata alama 0 hadi 2. Kwa

ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani wanafunzi 905,034 (59.14%) tu ndio waliopata alama kuanzia 4 hadi 12. Chati Na.2 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2*

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unadhihirisha kuwa, wanafunzi 122,790 (8.03%) walijibu vipengele vyote sita kwa usahihi na kupata alama zote 12 katika swali hili. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya umahiri mahususi wa Kutumia elimu ya hali ya hewa katika shughuli ya kila siku hivyo, waliweza kuoanisha kwa usahihi kati ya kazi za vifaa vya kupimia hali ya hewa na vifaa husika.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi walipata alama za juu katika swali hili kwa sababu walielewa vizuri matakwa ya swali katika kila kipengele.

Kipengele cha (i), mwanafunzi alitakiwa kutambua kifaa sahihi kinachotumika kupima mwanga wa jua. Jibu sahihi lilikuwa ni *H, Kampbeli Stok.* Jibu hili lilijibiwa na wanafunzi wenye uelewa wa kutosha kuhusu kazi ya Kampbeli Stok kama kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua. Wanafunzi waliochagua majibu mengine kama *A. Kipima joto* na *D. Barometa* hawakuwa na uelewa kuhusu kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa kipima joto ni kifaa kinachotumika kupima jotoridi na barometa hutumika kupima mgandamizo wa hewa.

Vilevile, katika kipengele cha (ii) mwanafunzi alitakiwa kutambua kifaa kinachotumika kupima jotoridi. Jibu sahihi lilikuwa ni *A, Kipimajoto.* Wanafunzi wenye maarifa ya kutosha kuhusu kazi ya Kipimajoto waliweza kujibu swali hili kwa usahihi. Aidha, wanafunzi wengine waliooanisha kipengele hiki na kipotoshi *E, Anemomita* walishindwa kuelewa kwamba Anemomita ni kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo. Hata hivyo, wanafunzi wengine walioanisha kipengele hiki na kipotoshi *C, Haigromita*. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa haigromita ni kifaa kinachotumika kupima unyevuanga.

Kipengele cha (iii) kilimtaka mwanafunzi kutambua kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa. Jibu sahihi lilikuwa ni *D, Baromita.* Wanafunzi wenye ujuzi na maarifa yakutosha kuhusu vifaa mbalimbali vinavyopima hali ya hewa walichagua jibu sahihi. Aidha, wanafunzi waliojibu kwa kuandika *H, Kampbeli Stok* hawakuelewa kuwa Kampbeli Stok ni kifaa kinachotumika

kupima mwanga wa jua. Hata hivyo, wanafunzi waliooanisha kipengele hiki na kipotoshi *F, Kipimaupepo* hawakuelewa kuwa kifaa hiki hutumika kupima uelekeo wa upepo na sio mgandamizo wa hewa.

Kipengele cha (iv) kilimtaka mwanafunzi kutambua kifaa kinachotumika kupima unyevuanga. Jibu sahihi lilikuwa ni *C, Haigromita.* Jibu hili lilijibiwa na wanafunzi wenye uelewa wa kutosha kuhusu kazi ya Haigromita kama kifaa kinachotumika kupima unyevuanga. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliooanisha kipengele hiki na kipotoshi *D, Baromita* hawakuelewa kuwa Baromita ni kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa.

Katika kipengele cha (v), mwanafunzi alitakiwa kutambua kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo. Jibu sahihi lilikuwa ni *E, Anemomita.* Jibu hili lilijibiwa na wanafunzi wenye uelewa wa kutosha kuhusu kazi ya Anemomita kama kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo. Hata hivyo, wanafunzi wengine walioanisha kipengele hiki kwa kuandika kipotoshi *D, Baromita* hawakuelewa kuwa Baromita ni kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa na sio mwendokasi wa upepo. Vilevile, wanafunzi waliooanisha kipengele hiki na kipotoshi *F, Kipima upepo,* hawakutambua kuwa, kifaaa hicho hutumika kupima uelekeo wa upepo na sio mwendokasi wa upepo.

Katika kipengele cha (vi) mwanafunzi alitakiwa kutambua kifaa kinachotumika kupima uelekeo wa upepo. Jibu sahihi lilikuwa ni

*F, Kipimaupepo.* Wanafunzi wenye uelewa wa kutosha kuhusu kazi ya kipimaupepo waliweza kujibu kwa usahihi. Kwa upande mwingine, wanafunzi wengine waliooanisha kipengele hiki na kipotoshi *D, Baromita,* wanafunzi hao hawakuelewa kuwa Baromita hutumika kupima mgandamizo wa hewa na sio uelekeo wa upepo. Kielelezo Na.1.1 na 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi na yasiyo sahihi ya wanafunzi katika swali la 2.

2. Jibu kipengele cha (i) - (vi) kwa kuoanisha kazi ya vifaa vya kupima hali ya hewa katika **Orodha A** na vifaa husika katika **Orodha B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| Orodha A | Herufi | Orodha B |
|---|---|---|
| (i) Kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua. | ( H ) | A Kipimajoto |
| (ii) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi. | ( A ) | B Kipima mvua |
| (iii) Kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa. | ( D ) | C Haigromita |
| (iv) Kifaa kinachotumika kupima unyevuanga. | ( C ) | D Baromita |
| (v) Kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo. | ( E ) | E Anemomita |
| (vi) Kifaa kinachotumika kupima uelekeo wa upepo. | ( F ) | F Kipimaupepo |
| | | G Stevenson screen |
| | | H Kampbeli Stok |

**Kielelezo Na.1.1:** *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote sita vya swali la 2*

2. Jibu kipengele cha (i) - (vi) kwa kuoanisha kazi ya vifaa vya kupima hali ya hewa katika **Orodha A** na vifaa husika katika **Orodha B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| Orodha A | Herufi | Orodha B |
|---|---|---|
| (i) Kifaa kinachotumika kupima mwanga wa jua. | ( D ) | A Kipimajoto<br>B Kipima mvua |
| (ii) Kifaa kinachotumika kupima jotoridi. | ( C ) | C Haigromita |
| (iii) Kifaa kinachotumika kupima mgandamizo wa hewa. | ( E ) | D Baromita<br>E Anemomita |
| (iv) Kifaa kinachotumika kupima unyevuanga. | ( A ) | F Kipimaupepo<br>G Stevenson screen |
| (v) Kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo. | ( H ) | H Kampbeli Stok |
| (vi) Kifaa kinachotumika kupima uelekeo wa upepo. | ( G ) | |

**Kielelezo Na. 1.2:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi ambaye alishindwa kuoanisha vipengele vyote katika swali la 2*

## 2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ya majibu mafupi, swali la 3 na la 4. Katika swali la 3 mwanafunzi alitakiwa kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yanayotokana na kifungu hicho. Swali hili lilikuwa na vipengele saba kila kimoja kilikuwa na alama 2 hivyo kufanya jumla ya alama 14. Katika swali la 4, mwanafunzi alitakiwa kusoma mchoro wa mfumo wa jua kisha aandike majina sahihi ya vitu vilivyopewa herufi A – D katika kipengele cha (i) – (iv). Kila kipengele kilikuwa na alama 2, hivyo jumla ya alama

katika swali la 4 zilikuwa 8. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa ufaulu katika swali la 3 na la 4 ulikuwa wa wastani.

### 2.2.1 Swali la 3: Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji mali

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *kufuata kanuni za uchumi katika shughuli za uzalishaji mali,* na umahiri mahususi wa *Kuthamini na kulinda rasilimali za nchi.* Katika swali hili, mwanafunzi alitakiwa kusoma habari kuhusu rasilimali za kijiji kisha kujibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

   Katika kijiji chetu tuna rasilimali kama vile maduka, nyumba na vyombo vya usafiri. Vilevile tuna misitu, mifugo, madini na ardhi. Rasilimali hizi hutumika kwa namna mbalimbali. Kwa mfano, vitu kama duka na mashamba hutupatia ajira na kutuongezea kipato cha familia. Misitu hutupatia dawa za asili ambazo hutibu magonjwa ya binadamu. Hali kadhalika, misitu husaidia kufanyika kwa mvua ambayo ni muhimu kwetu. Mazao yetu huhitaji mvua ili yakue. Pia, misitu hutupatia mbao kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zetu. Pia, misitu hutupatia kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia. Ardhi yenye uoto wa asili hutupatia maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo yetu. Mifugo hutupatia nyama, maziwa na mbolea na vyote hivi vinaweza kuuzwa na kuchangia kuongeza kipato cha familia.

**Maswali**

(a) Kwa namna gani wanakijiji hunufaika na rasilimali zilizopo?
(i) ______________________________
(ii) ______________________________

(b) Misitu ina umuhimu gani kwa wanakijiji?
(i) ______________________________
(ii) ______________________________

(c) Kwa nini mvua ni muhimu kwa mazao?
______________________________

(d) Uoto wa asili una umuhimu gani kwa wanyama?
______________________________

(e) Kutokana na habari, upi ni umuhimu wa mbao kwa wanakijiji?
______________________________


(f) Ni kwa namna gani mifugo huchangia kipato cha familia?
(i) ______________________________
(ii) ______________________________

(g) Wanakijiji wanatumiaje kuni wanazotoa msituni?
______________________________

**Kielelezo Na. 2.1***: Kifungu cha habari na maswali ambayo mwanafunzi alitakiwa kujibu katika swali la 3*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, swali hili lilijibiwa na jumla ya wanafunzi 1,530,381 (100%). Kati yao, wanafunzi 140,845 (9.20%) walikuwa na ufaulu mzuri sana kwani walipata alama zote

14. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kwani walijibu vipengele vyote 7 kwa usahihi. Wanafunzi wengine 476,134 (31.11%) walipata alama 10 hadi 12 ambao ni ufaulu mzuri. Wanafunzi hao walijibu kwa usahihi vipengele 5 hadi 6. Kwa upande mwingine, wanafunzi 388,814 (25.41%) walipata alama 6 hadi 8 ambao ni ufaulu wa wastani. Hata hivyo, wanafunzi 524,588 (34.28%) walipata alama 0 hadi 4 ambao ni ufaulu hafifu. Baadhi ya wanafunzi hawakujibu kipengele chochote au walijibu kwa usahihi kipengele 1 au 2. Kwa ujumla, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani jumla ya wanafunzi 1,005,793 (65.72%) walipata kuanzia alama 6 hadi 14. Chati Na. 3 inaonesha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Wanafunzi katika swali la 3*

Kipengele (a) mwanafunzi alitakiwa kubaini faida mbili zinazopatikana kutokana na rasilimali zilizopo kijijini ili kuwanufaisha wanakijiji kwenye habari aliyoisoma. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi waliweza kutaja faida mbili zinazopatikana kutokana na rasilimali zilizopo kijijini ambazo huchangia upatikanaji wa ajira na kuongeza kipato katika familia. Huu ni uthibitisho kuwa wanafunzi hao walisoma na kuelewa vizuri maudhui ya kifungu cha habari.

Aidha, baadhi ya wanafunzi waliandika majibu kama vile; *duka, ardhi, na hewa nzuri.* Wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika usomaji wa kifungu cha habari. Sambamba na hilo, wanafunzi wachache waliandika sentensi kama vile; *misitu, nyumba, magari na madini* ambayo si majibu sahihi. Majibu hayo yanathibitisha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na stadi ya kusoma kwa ufahamu kwani walishindwa kuelewa maudhui ya habari.

Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kubaini faida mbili za misitu kwa wanakijiji kutokana na habari aliyoisoma. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri, kwani wanafunzi wenye maarifa yakutosha waliweza kujibu kwa usahihi kwa kuandika umuhimu wa misitu kwa wanakijiji ambao ni, *kusaidia kufanyika kwa mvua* na *huwapatia wanakijiji dawa, kuni, mkaa na mbao.* Wanafunzi hao walionesha uelewa wa kusoma kwa ufahamu kifungu walichopewa.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wachache walikosa kipengele hiki kwa kuandika majibu yasiyo sahihi kama; *kupata matunda, kuvutia watalii* na *kupata hewa safi* Majibu hayo yanathibitisha kuwa wanafunzi katika kundi hili hawakuelewa matakwa ya swali hivyo waliandika majibu ambayo hayapo kwenye habari.

Katika kipengele (c) kilimtaka mwanafunzi kubaini umuhimu wa mvua kwa mazao kutokana na habari aliyoisoma. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri ambapo wanafunzi wengi waliweza kutaja kwa usahihi umuhimu wa mvua kwa mazao, kuwa ni *mazao huhitaji mvua ili yakue*. Kwa upande mwingine wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi kama vile; *kutupatia vyakula*, *kutupatia mashamba* na *kutupatia mbolea*. Majibu hayo yanathibitisha kuwa wanafunzi hawa hawakuelewa matakwa ya swali hivyo walinakili baadhi ya maneno au sentensi kutoka kwenye habari na kuandika kama majibu.

Katika kipengele (d) kilimtaka mwanafunzi kubaini umuhimu wa uoto wa asili kwa wanyama kutokana na habari aliyoisoma. Ufaulu katika kipengele hiki ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wenye maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa uoto wa asili kwa wanyama walijibu kwa usahihi kwa kuandika; *kuwapatia malisho wanyama.* Jibu hili, linaonesha kwamba wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusoma habari na kubaini ujumbe uliomo. Hata hivyo, wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu utunzaji wa uoto wa asili ambao huwezesha upatikanaji wa malisho kwa mifugo.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi katika swali hili waliandika majibu kama vile; *hutupatia dawa za asili kwa ajili ya kutibu magonjwa ya binadamu*, na *hutupatia kuni kwa ajili ya kupikia*. Wanafunzi hao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na kuandika majibu ambayo sio sahihi. Majibu haya yanathibitisha kwamba wanafunzi hawa hawakuwa na ujuzi wa kusoma na kuhusianisha dhana walioulizwa.

Kipengele hiki (e), kilimtaka mwanafunzi kubaini umuhimu wa mbao kwa wanakijiji kutokana na habari. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani, wanafunzi wengi walijibu kwa kuandika jibu sahihi ambalo ni *husaidia katika ujenzi wa nyumba.* Wanafunzi hao walikuwa na uelewa sahihi kuhusiana na matumizi ya mbao kuwa hutumika katika ujenzi wa nyumba.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walikuwa na ufaulu hafifu katika kipengele hiki. Wanafunzi hao walishindwa kubaini umuhimu wa mbao na kuandika majibu kama vile; *hutumika kutengeneza dawa* na *hutumika kupikia.* Majibu haya uonesha kuwa wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kusoma habari na kuhusianisha na dhana walioulizwa.

Kipengele (f) kilimtaka mwanafunzi kubainisha faida mbili ambazo mifugo huchangia kuongeza kipato cha familia kutokana na habari aliyoisoma. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani wanafunzi wengi walitoa jibu sahihi kuwa mifugo huchangia kuongeza kipato cha familia kwa; kuuza *maziwa*, *nyama* na


*mbolea*. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hawa walikuwa na maarifa ya kutosha katika kusoma habari na kuhusianisha na dhana walizoulizwa.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walishindwa kujibu kipengele hiki na kuandika majibu yasiyo sahihi. Waliandika; *misitu hutupatia dawa za asili, misitu husaidia kufanyika kwa mvua* na *mazao huhitaji mvua ili yakue.* Wanafunzi hao walinakiri baadhi ya maneno au sentensi kutoka kwenye habari ambayo hayaendani na matakwa ya swali. Majibu hayo yanathibitisha kuwa wanafunzi katika kundi hili hawakuwa na stadi ya kusoma kwa ufahamu.

Katika kipengele (g), mwanafunzi alitakiwa kubaini namna ambavyo wanakijiji wanazitumia kuni wanazozitoa msituni kama ilivyoelezwa kwenye habari aliyoisoma. Kipengele hiki kilijibiwa vizuri kwani wanafunzi wengi waliweza kuandika jibu sahihi kuwa ni *kwa ajili ya kupikia.* Wanafunzi hao walikuwa na maarifa na ujuzi wa kutambua matumizi ya kuni zinazopatikana msituni kwa wanakijiji.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walishindwa kuelewa matakwa ya kipengele hiki hivyo kuandika majibu yasiyo sahihi kama vile *kwa kukata mbao*, *kuchoma mkaa*, na *kutuongezea kipato.* Wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kusoma habari na hivyo kushindwa kubaini matumizi sahihi ya kuni zinazotoka msituni kama ilivyobainishwa katika habari waliyoisoma.

Vielelezo Na. 2.2 na 2.3 Sampuli ya majibu sahihi na yasiyo sahihi katika swali la 3.



**Maswali**

(a) Kwa namna gani wanakijiji hunufaika na rasilimali zilizopo?

(i) hutupatia ajira.

(ii) hunufaika kwa kipato.

(b) Misitu ina umuhimu gani kwa wanakijiji?

(i) kutupatia dawa za asili za binadamu.

(ii) Misitu husaidia kufanyika kwa mvua.

(c) Kwa nini mvua ni muhimu kwa mazao?

Mazao yanahitaji mvua ili kuweza kukua vizuri.

(d) Uoto wa asili una umuhimu gani kwa wanyama?

Kuna wanyama chakula chao ni majani.

(e) Kutokana na habari, upi ni umuhimu wa mbao kwa wanakijiji?

Ni ujenzi wa nyumba zao.

(f) Ni kwa namna gani mifugo huchangia kipato cha familia?

(i) Kwa kuuza nyama zao na kupata kipato.

(ii) Mbolea inayotokana na mifugo hutusaidia katika kilimo.

(g) Wanakijiji wanatumiaje kuni wanazotoa msituni?

kupikia

**Kielelezo Na. 2.2:** *Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 3*

**Maswali**

(a) Kwa namna gani wanakijiji hunufaika na rasilimali zilizopo?

(i) misitu

(ii) maziwa

(b) Misitu ina umuhimu gani kwa wanakijiji?

(i) kulima shamba

(ii) tupate mbolea

(c) Kwa nini mvua ni muhimu kwa mazao?

kutupatia hewa

(d) Uoto wa asili una umuhimu gani kwa wanyama?

uchomaji wa misitu

(e) Kutokana na habari, upi ni umuhimu wa mbao kwa wanakijiji?

Hutupatia mkaa

(f) Ni kwa namna gani mifugo huchangia kipato cha familia?

(i) Hutupatia maliho

(ii) Huongeza kipato cha familia

(g) Wanakijiji wanatumiaje kuni wanazotoa msituni?


maliko ya mifugo yetu

**Kielelezo Na.2.3:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali la 3*

### 2.2.2 Swali la 4: Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku* na katika umahiri mahususi wa *Kufahamu mfumo wa jua*. Swali hili lilimtaka mwanafunzi kusoma mchoro wa mfumo wa jua kisha kuandika majina sahihi ya vitu vilivyopewa hefupi A-D katika kipengele (i) – (iv). Swali liliuliza

4. Soma mchoro wa mfumo wa jua kisha andika majina sahihi ya sayari zilizopewa herufi A – D katika kipengele (i) – (iv).





(i) A____________________________

(ii) B____________________________

(iii) C____________________________

(iv) D____________________________

Jumla ya wanafunzi 1,530,381 (100%) walijibu swali hili. Kati yao, wanafunzi 857,146 (56.01%) walipata 0 hadi alama 2, ambao ni ufaulu hafifu. Wanafunzi 228,716 (14.94%) walipata alama 4 ambao ni ufaulu wa wastani. Wanafunzi wengine 144,907 (9.47%) walipata alama 6 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa upande mwingine wanafunzi 299,612 (19.58%) walipata alama zote 8 ambao ni ufaulu mzuri sana. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani jumla ya wanafunzi 673,235 (43.99%) walipata kuanzia alama 4 hadi 8. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4*

Uchambuzi zaidi unadhihirisha kuwa, wanafunzi 857,146 (56.01%) walipata alama 0 hadi 2 kwani hawakuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha kuhusu *Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku*. Wanafunzi hao walijibu swali hili kwa

kuandika majibu yasiyo sahihi kama yalivyoelezewa katika kila kipengele.


Katika kipengele cha (i) wanafunzi walitoa majibu yasiyo sahihi kama vile Dunia, Zuhura na *Sumbula*. *Wanafunzi hawa* walikosa ujuzi na maarifa ya kutambua kuwa kitu kikubwa kwenye mfumo wa jua ndio huwakilisha Jua.

Kipengele cha (ii), wanafunzi ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na mfumo wa jua walitoa majibu yasiyo sahihi, kama vile; *Zuhura*, *Zebaki* na *Jua.* Wanafunzi hawa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mpangilio wa sayari na vitu vyote vinavyounda mfumo wa jua.

Katika kipengele cha (iii) baadhi ya wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi kama vile; *Mirihi, Zohari* na *Kausi* Wanafunzi hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mpangilio wa sayari na vitu vinavyounda mfumo wa jua. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kuwa Mirihi ni sayari ya nne kutoka kwenye Jua, Zohari ni ya saba wakati Kausi ni sayari ya nane.

Katika kipengele cha (iv) baadhi ya wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi kama vile; *Sumbula, Zuhura* na *Kausi.* Wanafunzi hawa walikosa maarifa kuhusu mpangilio wa sayari na vitu vinavyounda mfumo wa jua hasa katika kuhusianisha nafasi zake kutoka kwenye Jua. Wanafunzi hao walipaswa kuelewa kwamba Sumbula ni sayari ya tano, Zuhura ni ya pili wakati Kausi ni sayari ya nane kutoka kwenye Jua. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu yasiyosahihi ya mwanafunzi katika swali la 4.

4. Soma mchoro wa mfumo wa jua kisha andika majina sahihi ya sayari zilizopewa herufi A – D katika kipengele (i) – (iv).




(i) A ______Kusini______

(ii) B ______MagaRiBi______

(iii) C ______MashaRiKi______

(iv) D ______KA SiKazini______

**Kielelezo Na. 3.1:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 4*

Katika Kielelezo Na. 3.1 mwanafunzi alitaja pande kuu za dunia badala ya vitu vinavyounda mfumo wa Jua.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 673,235 (43.99%) walipata alama kuanzia 2 hadi 8. Miongoni mwao, wanafunzi 299,612 (19.58%) waliopata alama 8 kwani walijibu kwa usahihi vipengele vyote. Wanafunzi hao walikuwa na maarifa yakutosha katika kufahamu mfumo wa jua. Vilevile wanafunzi 144,907 (9.47%)

waliopata alama 6 kwani walijibu kwa usahihi vipengele vitatu. Wanafunzi 228,716 (14.94%) waliopata alama 4 kwa kuwa walijibu kwa usahihi vipengele viwili tu. Majibu ya wanafunzi katika vipengele hivyo yalikuwa kama ifuatavyo:


Katika kipengele cha (i), mwanafunzi alitakiwa kubaini jina la kitu kilichooneshwa kwa herufi A. Jibu sahihi lilikuwa ni *Jua.* Wanafunzi waliotoa jibu sahihi katika kipengele hiki walikuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha kuhusu mfumo wa jua. Hivyo, waliweza kubaini kuwa herufi A imewakilisha kitu kikubwa kuliko vingine ambacho ni Jua katika mchoro wa mfumo wa Jua waliopewa.

Kipengele cha (ii) kilimtaka mwanafunzi kubaini jina la sayari iliyooneshwa kwa herufi B. Jibu sahihi lilikuwa ni *Dunia*. Wanafunzi waliotoa jibu sahihi katika kipengele hiki walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mfumo wa jua. Hivyo waliweza kubaini kuwa herufi B iliwakilisha sayari ya tatu ambayo ni *Dunia* katika mchoro wa mfumo wa jua waliopewa.

Katika kipengele cha (iii), mwanafunzi alitakiwa kubaini jina la sayari iliyooneshwa kwa herufi C. Jibu sahihi lilikuwa ni *Sumbula.* Wanafunzi waliotoa jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mfumo wa jua kwani waliweza kupanga sayari kwa usahihi na kubaini kuwa herufi C iliwakilisha sayari ya tano ambayo ni *Sumbula* katika mchoro wa mfumo wa jua waliopewa.

Kipengele cha (iv), mwanafunzi alitakiwa kubaini jina la sayari iliyooneshwa kwa herufi D. Jibu sahihi lilikuwa ni *Sarateni.* Wanafunzi waliotoa jibu sahihi katika kipengele hiki walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mpangilio sahihi wa sayari katika mfumo wa jua. Wanafunzi hawa waliweza kubaini kuwa herufi D iliwakilisha sayari ya sita ambayo ni *Sarateni.* Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 4.

4. Soma mchoro wa mfumo wa jua kisha andika majina sahihi ya sayari zilizopewa herufi A – D katika kipengele (i) – (iv).




(i) A *Jua*

(ii) B *Dunia*

(iii) C *Sumbula*

(iv) D *Sarateni*

**Kielelezo Na. 3.2:** *Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 4*

## 3.0 TATHIMINI YA UFAULU KWA KILA UMAHIRI

Uchambuzi katika Upimaji wa Darasa la Nne (SFNA) 2024 unaonesha kuwa, kati ya umahiri mkuu wa aina nne uliopimwa (kama ulivyoainishwa kwenye muhtasari wa Elimu ya Msingi wa somo la Maarifa ya Jamii wa mwaka 2016, kiwango cha ufaulu kilikuwa wastani katika umahiri wote uliopimwa. Umahiri uliofanya vizuri zaidi ni *Kufuata Kanuni za Kiuchumi katika Shughuli za Uzalishaji Mali* ulikuwa ni wa wastani kwa asilimia 65.72, *Kutambua Misingi ya Uzalendo katika Jamii* ulikuwa na ufaulu wa wastani asilimia 61.58, *Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka* ambao ulikuwa na ufaulu wa asilimia 59.14 na Umahiri wa Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku ulikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 43.99. Kwa upande mwingine, kiwango cha ufaulu katika umahiri wa Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku hakikuwa cha kuridhisha kwani wanafunzi wengi walikuwa na mapungufu yaliyosababisha kupata alama chache katika umahiri huo. Kiambatisho cha pekee kinaonesha mchanganuo wa kiwango cha ufaulu katika kila umahiri.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne 2024 katika somo la Maarifa ya Jamii umeonesha kiwango cha ufaulu cha wastani katika umahiri wote. Hata hivyo kuna changamoto zilizosababisha baadhi ya wanafunzi wasiwe na ufaulu mzuri katika umahiri wa Kutumia

Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku. Changamoto hizo ni pamoja na kushindwa kuelewa matakwa ya swali, kukosa maarifa katika dhana zilizopimwa na kushindwa kuwasilisha hoja katika mtiririko mzuri. Hata hivyo, wanafunzi waliokuwa na umahiri waliweza kubaini majibu sahihi katika maswali yaliyoulizwa na hivyo kuwa na ufaulu mzuri.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Wanafunzi wapewe mazoezi ya kutosha kuhusu mfumo wa jua kwa kuchora na kubainisha vitu vyote vinavyounda mfumo wa jua ili kuwajengea uelewa katika umahiri wa Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya Kila Siku.

(b) Wanafunzi wapatiwe fursa ya kufanya ziara za kimasomo maeneo mbalimbali ya kihistoria na Bunge ili kuwajengea umahiri wa Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii.

(c) Wanafunzi wapatiwe shughuli nyingi zitakazowasaidia katika upimaji wa stadi za kusoma na kuandika. Kwa mfano kupewa mazoezi ya kusoma matini na kuelezea ujumbe uliopo katika matini hizo. Hii itawasaidia wanafunzi walio na ujuzi mdogo wa kusoma na kuelewa maudhui mbalimbali.

(d) Wanafunzi wahimizwe kusoma vitabu vya kiada na ziada ili kuongeza maarifa na ujuzi ambao utawawezesha kujibu maswali ya upimaji kwa usahihi.

**KIAMBATISHO**

## 03 Maarifa ya Jamii: Ulinganifu wa Ufaulu kwa Wanafunzi katika kila Umahiri kwa Mwaka 2024 na 2023

| Na. | Umahiri | UPIMAJI 2024 | | | | UPIMAJI 2023 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu wa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu wa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya Swali | % ya ufaulu | | | Namba ya Swali | % ya Ufaulu | | |
| 1 | Kufuata Kanuni za Kiuchumi Katika Shughuli za Uzalishaji Mali | 3 | 65.72 | 65.72 | Wastani | 1 | 51.79 | 51.79 | Wastani |
| 2 | Kutambua Misingi ya Uzalendo Katika Jamii | 1 | 61.58 | 61.58 | Wastani | 2 | 29.79 | 29.79 | Hafifu |
| 3 | Kutambua Matukio Yanayotokea katika Mazingira Yanayomzunguka | 2 | 59.14 | 59.14 | Wastani | 3 | 66.83 | 66.83 | Wastani |
| 4 | Kutumia Ramani na Elimu ya Anga katika Maisha ya kila Siku | 4 | 43.99 | 43.99 | Wastani | 4 | 57.76 | 57.76 | Wastani |